

Maambukizi yaliyofichika ya kifua kikuu - wakati matibabu yanapotolewa

Taarifa kwa mgonjwa kutoka kwa daktari wa magonjwa ya kuambukiza nchini Uswidi.

Kwa nini nimepokea taarifa hii?

Kipimo kimeonyesha kwamba una maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika. Daktari wako anaona kwamba unahitaji matibabu ili kupunguza hatari ya kuugua kifua kikuu baadaye.

Hapa kuna taarifa ya mambo ya kuzingatia.

Maambukizi yaliyofichika ya kifua kikuu ni nini?

Maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika yanamaanisha kwamba umeambukizwa bakteria za kifua kikuu, lakini huna ugonjwa kutokana nayo. Mtu anapoambukizwa bakteria za kifua kikuu, mfumo wa kinga ya mwili huitikia na hii inaweza kupimwa kwa kipimo cha damu au kipimo cha ngozi. Watu wengi walioambukizwa huendelea kuwa na afya njema, lakini kuna hatari ndogo ya kuugua kifua kikuu baadaye maishani.

Hatari ya kuugua baadaye ni kubwa zaidi kwa watu walioambukizwa hivi karibuni, kwa wajawazito, wale ambao wametoka kujifungua, watoto, vijana na kwa watu walio na kinga dhaifu kutokana na ugonjwa au matibabu ya dawa.

Je, maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika yanaambukiza?

Hapana, maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika hayaambukizi. Kifua kikuu kinaweza kuambukiza tu wakati mtu ni mgonjwa na ugonjwa wa kifua kikuu uko kwenye mapafu.

Je, ninahitaji matibabu ya maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika?

Ndiyo, daktari wako anatathmini kwamba unahitaji matibabu ili kupunguza hatari ya wewe kuugua kifua kikuu baadaye.

Ninapaswa kuzingatia nini?

Hakuna njia ya kupima kama bakteria zote zimetoweka baada ya matibabu na unaweza kuambukizwa tena katika siku zijazo.

Ikiwa katika siku zijazo utapata matatizo ya muda mrefu (zaidi ya wiki tatu) kama kikohozi, homa, jasho la usiku au kupungua uzito bila kukusudia, unapaswa kuwasiliana na daktari. Sema kwamba hapo awali umepokea matibabu ya maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika.

Taarifa ya mawasiliano (Kontaktuppgifter)

Kitengo cha matibabu (Mottagning).....

.....

Simu (Telefon).....